sekretarieti ya maadili

# Jarida la MAADILI

Toleo la 05: Aprili- Juni 2025

www.maadili.go.tz

**DIRA:UADILIFU KWA VIONGOZI WA UMMA**



Scan kusoma
Jarida Kidijitali

## MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA Dkt. SAMIA

**Mambo Nane Yaguswa Ndani ya Sekretarieti ya Maadili** *Inaendelea UK..5*

# Y A L I Y O M O


**Ukurasa wa 2**
**Yaliyomo**

**Ukurasa wa 3**
**Tahariri**



**Ukurasa wa 4 na 6**
Maadili na IAA Wazindua Hati ya Makubaliano ya Kukuza Maadili



**Ukurasa wa 5, 7, 12, 13 na 21**
Mafanikio ya Miaka Minne ya Dkt. Samia Mambo Nane Yaguswa Sekretarieti ya Maadili.



**Ukurasa wa 8 , 9, 17, 19, 20 na 22**
**Habari Picha**



**Ukurasa wa 10, 11 na 18**
Sekretarieti ya Maadili Yawapiga Msasa Viongozi wa Kanda za Ziwa na Kati.

**Ukurasa wa 14, 15 na 16**
Viongozi wa Umma wafurahia Ujazaji wa Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya Mtandao


## WAJUMBE WA BODI YA UHARIRI


| | |
|---|---|
| Bw. Honoratus Ishengoma | Mwenyekiti |
| Bi. Johanither Barongo | Katibu |
| Bi. Grace Mariki | Mjumbe |
| Bw. Baraka Mwashambwa | Mjumbe |
| Bw. Godfrey Mbai | Mjumbe |

# TAHARIRI

# Matumizi ya ODS Yawaondolea Adha Viongozi wa Umma

Katika miaka ya hivi karibuni Serikali imefanya mabadiliko makubwa ya utoaji huduma kwa wananchi wake kwa kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Matumizi ya TEHAMA yameleta matokeo chanya katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa kuondoa uwezekano wa mtoaji na mpokeaji huduma kukutana ana kwa ana na hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma na kuondoa vishawishi.

Katika matumizi ya mifumo hiyo, tumeshuhudia mara kadhaa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba zake mbali mbali, akisisitiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA na kuagiza kuwa ifikapo Desemba, 2024 mifumo ya Serikali isomane kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi na kuongeza tija.

Sio siri kwamba dunia imebadilika na matumizi ya mifumo hiyo haiepukiki. Kumekuwepo na faida nyingi kwa watumiaji wa mifumo ya TEHAMA ikilinganishwa na analojia. Baadhi ya faida hizo ni kupunguza gharama, kuokoa muda, kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kupunguza mikutano na mazungumzo ya ana kwa ana yaliyokuwa yakifanyika wakati wa upokeaji na utoaji huduma, kurahisisha mawasiliano na kuongeza usahihi wa kazi.

Kutokana na hali hiyo, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma tangu mwaka 2023 ilianzisha matumizi ya Mfumo wa Ujazaji wa Tamko la Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma kwa njia ya Mtandao (Online Declaration System - ODS). Mfumo huu unamuwezesha Kiongozi wa Umma kujaza Tamko lake na kuliwasilisha kwa Kamishna wa Maadili akiwa mahali popote duniani ambapo mtandao unapopatikana.

Mfumo huu umeanzishwa ili kutekeleza Sera ya Serikali Mtandao (e – Government Policy) ambayo Serikali imeagiza Wizara, Idara na Taasisi zote za Umma kutumia mifumo ya TEHAMA katika kurahisisha mawasiliano na utendaji kazi Serikalini.

Matumizi ya ODS ni hatua kubwa katika safari yetu ya maboresho na ubunifu wa kidigitali wa kujenga mifumo ya kuwajali wadau wetu kwa kuwapunguzia adha ya kutumia gharama kubwa na muda mwingi kuwasilisha matamko yao kwa Kamishna wa Maadili.

ODS ina faida kubwa ikiliganishwa na njia iliyokuwa ikitumika awali. Mathalani, Sekretarieti ya Maadili ilikuwa ikitumia kati ya Shilingi milioni 35 hadi 40 kwa mwaka kuchapisha fomu za Tamko na kuwapelekea Viongozi wa Umma ili wazijaze na kuzirejesha kwa Kamishna wa Maadili. Baada ya kujaza Tamko, kiongozi alilazimika kusafiri umbali mrefu kuliwasilisha Makao Makuu ya Sekretarieti ya Maadili au katika ofisi zetu za Kanda. Utaratibu huu, ulikuwa ukiwaongezea Viongozi na Taasisi gharama kubwa za uendeshaji ambazo baada ya kuanzishwa kwa ODS zimeokolewa. Kwa sasa fedha hizo zinaelekezwa katika matumizi mengine ya maendeleo.

Mfumo wa ODS utawawezesha Viongozi kujaza matamko yao kwa urahisi na kwa usahihi zaidi popote pale watakapokuwa, iwe ndani au nje ya nchi.

ODS imempunguzia kiongozi muda wa kusafiri kwani anajaza Tamko lake na kuliwasilisha bila kuhitajika kusafiri. Utendaji kazi wa Taasisi umerahisishwa. Kazi ya kuchambua matamko inafanyika kwa usahihi na wepesi zaidi tofauti na kipindi cha matumizi ya nakala ngumu.

Aidha, matumizi ya ODS yanarahisisha utunzaji wa kumbukumbu na taarifa za Viongozi kwa kuondoa nakala ngumu (hard copy). Taarifa hizi zinabaki na ubora wake kwa muda mrefu tofauti na nakala ngumu.

Hadi tarehe 31 Desemba, 2024, jumla ya Viongozi wa Umma 15,480 waliwasilisha Tamko lao la mwisho wa mwaka kwa njia ya ODS. Hili ni jambo la kujivunia kuwa Viongozi wengi wameitikia wito na kutimiza takwa hili la kisheria.

Kwa nafasi hii, tunapenda kuwashukuru Viongozi wote wa Umma nchini kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Sekretarieti ya Maadili katika uteklezaji wa majukumu yake.

Sekretarieti ya Maadili itaendelea kutekeleza agizo la Serikali la kutumia mifumo ya TEHAMA kuwahudumia wadau ili kuleta ufanisi wa kazi na kuwaondolea changamoto ya matumizi ya fedha na muda.

Tunaamini Viongozi wa Umma wataendelea kutoa ushirikiano kwa kuwasilisha matamko yao kwa njia ya mtandao.

# Maadili na IAA Wazindua Hati ya Makubaliano ya Kukuza Maadili

Serikali ya Awamu ya Sita inazidi kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha uadilifu kwa kubuni mikakati itakayosaidia kutoa elimu ya maadili kwa viongozi na watumishi wa umma nchini ili waweze kuzingatia misingi ya maadili na uadilifu wanapotekeleza majukumu yao.

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na malalamiko kuhusu kuwepo kwa viashiria vya mmomonyoko wa maadili kwa baadhi ya viongozi na watumishi wa umma nchini. Baadhi ya viashiria hivyo ni mgongano wa maslahi, matumizi mabaya ya madaraka, vitendo vya rushwa na ubadhirifu.

Katika jitihada za kutatua changamoto hizo, tarehe 6 Machi, 2025 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliingia makubaliano ya ushirikiano na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) katika nyanja mbalimbali ikiwemo kutoa elimu ya maadili kwa viongozi na watumishi wa umma. Hati ya Makubaliano hayo ilizinduliwa jijini Dodoma na Mhe. George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kabla ya uzinduzi huo, Makamu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu, Arusha Dkt. Grace Idinga alieleza kuwa makubaliano yaliyofikiwa na pande mbili yanalenga kufanikisha mambo mbalimbali ikiwemo kuimarisha uwezo wa watumishi na viongozi wa umma kuhusu maadili, utawala bora, uadilifu wa kifedha na uwajibikaji.




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (Mb) akikata utepe kuzindua hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA). Kushoto kwa Waziri ni Kamishna wa Maadili Mhe. Jaji (Stahiki) Sivangilwa Mwangesi na kulia kwake ni Mkuu a Chuo cha IAA Prof. Eliamani Sedoyeka . Uzinduzi huo ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa PSSSF jijini Dodoma tarehe 6 Machi, 2025.*

Kutoa mafunzo kuhusu uzingatiaji wa maadili, kutoa ushauri wa kitaalamu, kufanya utafiti, kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, matumizi sahihi ya rasilimali na uchunguzi wa kitaaluma kuhusu utawala bora.

Katika makubaliano hayo, viongozi na watumishi wa umma watapatiwa mafunzo ya muda mfupi yatakayo jumuisha kada mbalimbali za uongozi. Kada hizo ni Makatibu Wakuu wa Wizara, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Maafisa Elimu, Wakuu wa Idara na Vitengo katika Taasisi za Umma pamoja na watumishi wa kada mbalimbali.

"Mafunzo yatakayotolewa, yatasaidia kupunguza mienendo isiyo ya kimaadili katika utumishi wa umma kwa kuwawezesha viongozi kufanya maamuzi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo," alisema.

Akizindua makubaliano hayo, Mhe. Simbachawene alipongeza ushirikiano huo na kusema, "Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambayo imejikita katika kuimarisha Maadili ya Viongozi, uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimali za umma ambayo pia ni hatua muhimu katika kutekeleza mikakati ya maendeleo ya Taifa."

"Suala la uadilifu katika uongo-

Inaendelea UK.....6

# Mafanikio ya Miaka Minne ya Dkt. Samia  Mambo Nane Yaguswa Sekretarieti ya Maadili



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwaaga wananchi mara baada ya kumaliza mkutano wa kuhitimisha ziara yake katika uwanja wa Majimaji, Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma tarehe 28 Septemba, 2024.*

Tangu Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani, suala la maadili limeendelea kuwekewa mkazo ili kujenga uadilifu, uwajibikaji, uwazi na usikivu miongoni mwa Viongozi na Watumishi wa Umma. Hatua hii ina lenga kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu kwa uadilifu, uaminifu na kukuza imani na heshima ya wananchi kwa Serikali.

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imepata mafanikio makubwa.

Mafanikio hayo yanatokana na utekelezaji wa jukumu la msingi la kuchunguza tabia na mwenendo wa Kiongozi wa Umma yeyote kwa mujibu wa Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398. Katika Awamu ya Sita, Sekretarieti ya Maadili ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake ya kisheria na kupata mafanikio yafuatayo;

Uhakiki wa fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni ni Moja kati ya kazi za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kufanya Uhakiki wa Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma. Uhakiki huo unafanyika ili kubaini usahihi wa taarifa za rasilimali na madeni zilizotamkwa na kiongozi wa umma na kujiridhisha kama kile kilichotamkwa ndicho anachomiliki. Aidha, uhakiki wa tamko hulenga kubaini utofauti kati ya rasilimali na madeni ya kiongozi kwa kulinganisha na vyanzo halali vya mapato.

*Inaendelea UK....7*

# Maadili na IAA wazindua Makubaliano ya Kukuza Maadili



*Viongozi mbalimbali wakifuatilia zoezi la uzinduzi wa Hati ya Makubaliano ya ushirikiano kati ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Chuo Cha Uhasibu Arusha (IAA). Uzinduzi huo ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa PSSSF jijini Dodoma tarehe 6 Machi, 2025.*

*Inatoka UK...4*

zi wa umma ni nguzo muhimu ya maendeleo ya Taifa lolote, hivyo viongozi wote na watumishi wa umma wanapaswa kuwa mfano bora wa uwajibikaji, uaminifu, na utendaji wa haki. Taifa lenye viongozi waadilifu linakuwa na Taasisi imara, zenye kuwahudumia wananchi kwa haki na usawa," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Simbachawene, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuhakikisha kuwa maadili ya utumishi wa umma yanazingatiwa ili kujenga imani kwa wananchi na kuimarisha utendaji wa Taasisi za Umma.

Na hapa naomba nimnukuu Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa, aliwahi kusema kuwa "Uongozi ni dhamana, na kila kiongozi anapaswa kuwa mtumishi wa watu, si mtawala wa watu."

Mhe. Waziri aliagiza Taasisi zote za Serikali kuhakikisha viongozi wake wanahudhuria mafunzo hayo ili yawajenge katika uadilifu na usimamizi bora wa rasilimali.

"Mafunzo haya ni fursa muhimu ya kuimarisha utendaji kazi wa viongozi na watumishi wa umma. Kupitia mafunzo haya, watakuwa na uelewa mpana wa misingi ya utawala bora na maadili na yataleta mabadiliko chanya katika Taasisi wanazoziongoza na Taifa," alisema.

Katika hatua nyingine, Mhe. Simbachawene alitoa rai kwa vyuo na Taasisi nyingine za elimu ya juu kuiga mfano huu kwa kushirikiana na Serikali kuimarisha mitaala inayohusiana na uadilifu, uwajibikaji na utawala bora.

Kwa upande wake Kamishna wa Maadili, Mhe. Jaji (Stahiki) Sivangilwa Mwangesi alisema Sekretarieti ya Maadili ina jukumu la kuhakikisha viongozi wa umma wanazingatia maadili katika utendaji wao wa kazi. "Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka mifumo thabiti ya kuhakikisha kuwa viongozi wanazingatia misingi ya uwajibikaji, uwazi na usimamizi wa rasilimali za umma kwa manufaa ya Taifa," alisema.

Katika maelezo yake ya utangulizi, Kamishna Mwangesi alisema kuwa uzingatiaji wa maadili na uongozi bora ni jukumu la pamoja linalohitaji ushirikiano wa wadau wote, zikiwemo taasisi za umma, sekta binafsi, asasi za kiraia na mashirika ya kimataifa.

"Kupitia ushirikiano huu ninaamini tunaweza kujenga mfumo imara wa maadili unaozingatia misingi ya haki, usawa na utawala bora. Mkakati huu wa kutoa elimu kwa viongozi na watumishi wa umma utaimarisha mifumo yetu ya uwajibikaji na kuondoa changamoto zilizopo," alisema.

# Mafanikio ya Miaka Minne ya Dkt. Samia

*Inatoka UK...5*

Katika kipindi cha miaka minne, idadi ya viongozi waliohakikiwa mali zao imeongezeka kutoka viongozi 3,119 mwaka 2020 hadi viongozi 4,961 kufikia Machi 2025. Uhakiki wa Tamko la Rasilimali na Madeni umebaini kuwepo na ongezeko la viongozi wa umma kuzingatia misingi ya Sheria ya Maadili kwa kuonesha uwazi kuhusu rasilimali na madeni wanazomiliki.

Kasoro na dosari katika matamko ya Viongozi wa Umma imepungua kutoka mwaka hadi mwaka, ikiashiria kuongezeka kwa uadilifu wa viongozi katika kutamka mali wanazomiliki na maslahi waliyonayo. Idadi ya viongozi ambao hawakuwa na dosari katika matamko yao imeongezeka kutoka asilimia chini ya 90 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 92 mwaka 2024.

Kwa upande wa uhakiki wa Tamko la mgongano wa maslahi, imebainika kuwa idadi ya viongozi waliokutwa na mgongano halisi wa maslahi imeendelea kupungua kutoka asilimia nane (8) mwaka 2021 hadi kufikia asilimia tatu (3) mwaka 2024. Hali hii inaashiria kuanza kuimarika kwa uadilifu na kupungua kwa vitendo vya migongano ya maslahi kwa viongozi wa umma.

### Kushughulikia Malalamiko ya Ukiukwaji wa Maadili

Katika kipindi hiki, Sekretarieti ya Maadili imeongeza kasi ya kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya viongozi wa umma. Malalamiko haya ni yale yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995. Wastani wa malalamiko yaliyopokelewa kila Mwaka (yanayohusu Sheria na yasiyohusu Sheria) ni 186 katika Awamu ya Sita ikilinganishwa na malalamiko 230 kwa Mwaka kati ya mwaka 2015-2020. Malalamiko hayo ni sawa na asilimia tano ya jumla ya viongozi wanaolalamikiwa ikilinganishwa na asilimia sita ya viongozi waliolalamikiwa kati ya mwaka 2015 hadi 2020. Takwimu hizi zinaonesha kuwa idadi ya viongozi wanaolalamikiwa imepungua kwa asilimia moja katika uongozi wa Awamu ya Sita. Kupungua kwa malalamiko kunatokana na elimu inayotolewa mara kwa mara na Sekretarieti ya Maadili kwa Viongozi wa Umma kuhusu Sheria ya Maadili.

Kupungua kwa malalamiko yanayohusu sheria hasa suala la uwajibikaji ni moja ya kiashiria kinachoonesha kukua kwa uadilifu miongoni mwa viongozi wa umma. Hata hivyo, kati ya aina 11 za malalamiko yaliyowasilishwa, aina nne (4) za

*Inaendelea UK...12*




*Mwenyekiti wa Baraza la Maadili Mhe. Jaji (Mst.) Rose Teemba (katikati), akiongoza kikao cha Baraza hilo kilichofanyika mwishoni mwa mwezi Machi ,2025 kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu jijini Dodoma.*

# HABARI PICHA



*Afisa Maadili Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati-Dodoma Bi. Deborah Mwanjali akipanda mche wa mti katika Sekondari ya Sejeli Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma katika zoezi la upandaji miti kwa shule wanachama wa klabu za maadili Kanda ya Kati iliyotolewa na Ofisi hiyo. Zoezi hilo lilifanyika shuleni hapo tarehe 19 Machi, 2025.*



*Baadhi ya Viongozi wa Umma walioshiriki mafunzo kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma wakimsikiliza mtoa mada Bw. Innocent Shetui (hayupo pichani). Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba tarehe 8 Mei, 2025.*



*Afisa wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati-Dodoma Bi. Philipina Kobelo (wa kwanza kushoto)) akitoa elimu ya maadili kwa Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Magereza CP. Nicodemus Tenga alipotembelea banda la ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 29 Januari, 2025.*



*Mkuu wa Shule ya Sekondari Sejeli Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma Bw. Otto Matandula akiongoza zoezi la upandaji miti iliyotolewa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati-Dodoma. zoezi hilo lilifanyika shuleni hapo tarehe 19 Machi, 2025.*

# Sekretarieti ya Maadili Yawapiga Msasa Viongozi wa Kanda ya Ziwa na Kati

Moja kati ya jukumu la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma na wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kutokana na sababu hiyo, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Ummakatika kipindii cha miaka mine (2022/26), iliweka kipaumbele kutoa elimu kwa umma ili kuimarisha dhana ya Uwajibikaji wa Pamoja kwa Viongozi wa Umma nchini hasa katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Lengo la elimu hiyo ni kuhamasisha utendaji kazi wa pamoja, kuwaelimisha viongozi wa um-ma kuepuka tabia ya kupingana hadharani, kuunga mkono maamuzi yanayofan-ywa na mamlaka za juu serikalini ikiwemo Kamati na Mabaraza ya Madiwani. Lengo jingine ni kuunga mkono sera za Serikali, kutunza siri za Serikali na kuzingatia mipaka ya majukumu ya kazi.

Elimu hii ambayo hadi sasa imetolewa katika Kanda zote nane za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imeanza kuleta manufaa kwani baadhi ya viongozi waliokuwa wakikinzana wameanza kufanya kazi kwa ushirikiano na kila mmoja kuheshimu mipaka yake ya kazi.

Kabla ya utoaji huo wa elimu, kulikuwa na tabia ya baadhi ya Viongozi wa Umma kukinzana hadharani katika kauli hasa katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

Kukinzana huku kunatokea kati ya viongozi, watendaji, waheshimiwa madiwani na wananchi. Tabia hii inasababisha migongano katika utendaji na kudhorotesha utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Migongano hii inatokana na baadhi ya viongozi wa umma kutokufahamu mipaka ya majukumu yao, upya wa baadhi ya viongozi, uelewa mdogo wa sheria mbalimbali zinazotawala utendaji kazi, umri mdogo na uzoefu katika uongozi.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, jumla ya viongozi wa umma 2,400 kutoka Halmashauri za Wilaya 44 nchini walipatiwa mafunzo ya Uwajibikaji wa Pamoja.

Sekretarieti ya Maadili katika mwaka wa fedha (2024/25) imeendelea kutoa elimu ya Uwajibikaji wa Pamoja kwa viongozi wa Kamati za Ushauri za mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Mara na Geita. Jumla ya viongozi wa umma 550 waliwudhuria mafunzo hayo kutoka mikoa hiyo miwili. Viongozi walioshiriki mafunzo hayo ni pamoja na Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara na Vitengo, Waheshimiwa Madiwani na Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa.



Aidha, katika Kanda ya Kati Dodoma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilifanikiwa kutoa mafunzo ya Maadili katika Halmashauri za Itigi, Mkalama, Chemba, Bahi, Chamwino na Singida ambapo jumla ya viongozi wapa-

*Inaendelea UK...11*

tao 683 walipewa mafunzo kuhusu sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa ujumla.

Mada zilizofundishwa na kujadiliwa na washiriki katika mafunzo hayo zilihusu uwajibikaji wa pamoja, Mgongano wa Maslahi pamoja na Ujazaji wa Tamko la Raslimali na Madeni kwa njia ya Mtandao. Mafunzo hayo yaliwashirikisha Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo katika Halmashauri hizo.

Katika Halmashauri hizo kulikuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo; Muingiliano kati ya Watendaji wa Kata, Vijiji na Madiwani katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri, kutoelewana kati ya Waheshimiwa Madiwani, Wakuu wa Idara na Watumishi kulikotokana na mgongano wa maslahi baina ya pande husika, Madiwani kuchochea migogoro kwa kuwalaumu wananchi kutoshiriki katika miradi ya maendeleo kutokana na uhusiano mbaya kati ya Madiwani na Watumishi wa Halmashauri.

Migogoro mingine inatokana na upya katika uongozi unaosababisha kukosa uelewa wa sheria, kanuni na taratibu na Wakuu wa Idara na Vitengo kutumia fursa ya uelewa mdogo wa Mkurugenzi kukiuka sheria, kanuni na taratibu.

Katika Halmashauri za mikoa ya Singida na Dodoma pia kulikuwa na baadhi ya Madiwani ambao hawakuwa na imani na Wakuu wa Idara na Vitengo kulikosababisha kutoshirikiana kuleta maendeleo na kuibua migogoro.

Akifungua mafunzo hayo kwa wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mara hivi karibuni mjini Musoma, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi alitoa wito kwa viongozi wa umma mkoani humo kuzingatia matakwa ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma wanapotekeleza majukumu yao.

"Mafunzo haya yana manufaa sana kwetu kwani yataongeza nidhamu na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu serikalini pia ni kielelezo cha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha kuwa suala la maadili na uwajibikaji linaeleweka kwa wadau wote wa sekta ya umma na sekta binafsi," alisema.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Mara, maadili yana umuhimu mkubwa katika kujenga imani ya wananchi kwa viongozi na serikali yao. Maadili pia yanaimarisha usimamizi bora wa raslimali za umma, utii wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, udhibiti wa mianya ya rushwa, kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa.

"Wapo baadhi ya viongozi wa

*Inaendelea UK...18*



***Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya maadili wakisikiliza hotuba ya Mgeni rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Martin Shigella (hayupo pichani) katika mafunzo ya maadili yaliyofanyika katika ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita tarehe 6 Machi 2025.***



*Viongozi mbalimbali walioapishwa wakitoa Ahadi ya Uadilifu katika moja ya zoezi la uapisho wa Viongozi wa Umma. Zoezi hilo liliongozwa na Kamishna wa Maadili Mhe. Jaji (Stahiki) Sivangilwa Mwangesi (hayupo pichani) Ikulu ndogo ya Tunguu, Zanzibar tarehe 10 Desemba, 2024.*

*Inatoka UK...7*

malalamiko zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara. Aina hizo ni uonevu, mgongano wa maslahi, matumizi mabaya ya madaraka na migogoro ya ardhi. Sekretarieti itaendelea kutoa elimu kwa Umma na hasa kwa Viongozi ili kupunguza malalamiko hayo hasa yale ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Kutoa Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya Mtandao.**

Katika awamu hii, urejesha wa Tamko kwa wakati umefikia asilimia 97 Desemba 31, 2024. Urejeshaji huo ni zaidi ya lengo la asilimia 95 lililowekwa katika Mpango Mkakati wa Taasisi.

Hali hii ya urejeshaji wa tamko kwa wakati imetokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha Viongozi wanafuata misingi ya Maadili.

Aidha, ni juhudi za Sekretarieti kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma kuhusu Sheria ya Maadili hususan umuhimu wa kutoa Tamko la Rasilimali na Madeni, kuwaandikia barua viongozi wanaochelewa kutoa Tamko kwa wakati na kuwataka watoe maelezo ya kina kuhusu sababu zilizowafanya wachelewe kutoa Tamko pamoja na kuanza matumizi ya Mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa Tamko kwa njia ya Mtandao (Online Declaration System - ODS) kumechangia mwitikio mkubwa wa urejeshaji wa Tamko la mwaka. ODS imewasaidia Viongozi wa Umma kujaza Tamko na kuliwasilisha kwa Kamishna wa Maadili wakiwa mahali popote penye mtandao.

Katika kipindi husika, viongozi ambao hawakutoa Tamko la mwisho wa mwaka la Rasilimali na Madeni kwa wakati, bila kuwa na sababu au maelezo ya msingi, walifikishwa mbele ya Baraza la Maadili kwa ajili ya uchunguzi wa kina. Jumla ya Viongozi saba walifikishwa mbele ya Baraza la Maadili kwa kosa la kutokutoa Tamko la Mwaka la Rasilimali na Madeni. Ilikuhakikisha viongozi wakidhi takwa hili la Sheria, Sekretarieti itaendelea na juhudi za kuwasiliana na mamlaka za uteuzi ili kuhakikisha Viongozi wote wanapata taarifa na elimu ya

*Inaendelea UK....13*

*Inatoka UK..12*

umuhimu wa kujaza tamko ili kukuza uadilifu.

Kimsingi, uadilifu katika eneo la utoaji wa Tamko kwa mwaka umeendelea kuimarika katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita. Pamoja na utoajii wa Tamko, uchambuzi unaonesha kuwa matamko yasiyo na kasoro yameendelea kuongezeka kutoka asilimia 85 mwaka 2021 hadi asilimia 87 mwaka 2024.

**Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Marekebisho ya Sheria yameongeza wigo wa viongozi wanaowajibika kwa mujibu wa Sheria na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Sekretarieti ya Maadili. Katika kipindi cha Awamu ya Sita, Serikali imefanya marekebisho makubwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yenye lengo la kuongeza ufanisi, kuimarisha na kukuza utawala bora na uwajibikaji wa viongozi kwa wananchi.

Katika kuiwezesha Sekretarieti ya Maadili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Serikali pia imewezesha kufanya urekebu na ujumuishaji wa marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hatua hii ililenga kuyaweka mabadiliko yote sehemu moja ili kurahisisha matumizi ya Sheria kwa wadau. Aidha, katika kipindi husika, Sekretarieti ya Maadili imetafsiri Sheria ya Maadili kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili kama Sheria ya Tafsiri za Sheria inavyoelekeza kuwa Sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ziwe katika lugha ya Kiswahili.

**Utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu na Hali ya Uadilifu Nchini**

Tangu Awamu ya Sita ilipoingia madarakani, kumekuwepo na ongezeko la uzingatia wa Masharti ya Hati ya Ahadi ya Uadilifu miongoni mwa Viongozi katika sekta za umma na binafsi. Hatua hii inachangia kukuza uadilifu katika sekta ya umma na binafsi nchini. Hatua hii inatokana na Ahadi ya Uadilifu kuainisha masuala muhimu ya kimaadili yanayotakiwa kuzingatiwa na Kiongozi wa Umma wakati akitekeleza majukumu yake. Viashiria vya uzingatiaji wa Ahadi ya Uadilifu vinaonesha kuwa katika Awamu ya Sita, malalamiko yanayohusu mgongano wa maslahi, rushwa na unyanyasaji yamepungua.

Katika kipindi cha 2020-2024, idadi ya viongozi waliosaini Hati za Ahadi ya Uadilifu imeongezeka kwa asilimia 13 kutoka viongozi 6,051 katika Awamu ya Tano hadi viongozi 6,862. Hati ya Ahadi ya Uadilifu husainiwa na Kiongozi mpya, aliyepata uteuzi, kupanda cheo au kubadilisha cheo. Kiongozi wa Umma anaposaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu ni ishara kuwa atazingatia masharti 12 yaliyowekwa katika hati hiyo.

Sekretarieti ya Maadili, itaendelea kutoa elimu ya Maadili kwa viongozi wa umma hususan Hati ya Ahadi ya Uadilifu ili kuimarisha misingi ya uadilifu. Aidha, Sekretarieti ya Maadili itaendelea kufuatilia Viongozi wa Umma ili kubaini viongozi wanaokiuka misingi ilibainishwa katika Hati ya Ahadi ya Uadilifu na kuchukua hatua stahiki.

**Mafunzo kuhusu Sheria ya Maadili**

Moja kati ya kazi zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni utoaji wa elimu kwa umma. Katika awamu hii, utoaji wa elimu kwa umma kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma umeongezeka.

Elimu hii imekuwa ikitolewa kwa njia mbalimbali zikiwemo; semina, mafunzo, maonesho ya wasanii, vipindi vya redio na luninga. Mathalani katika kipindi cha 2020-2024, Sekretarieti ya Maadili imekuwa na vipindi vya redio 470, luninga 20 na kuanzisha Klabu za Maadili 2,130 zenye wanachama zaidi ya 77,000 ukilinganisha na vipindi 160 (redio), 12 (luninga), Klabu 262 zenye Wanachama 10,034 tu mwaka 2020.

Aidha, Sekretarieti imezifikia Halmashauri 97 nchini ambapo jumla ya viongozi na watumishi wa umma 4,500 wamepatiwa mafunzo maalumu kuhusu Uwajibikaji wa Pamoja. Elimu imesaidia kupunguza idadi ya

*Inaendelea UK... 21*

# Viongozi wa Umma wafurahia Ujazaji wa Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya Mtandao




*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu (Mb) akizungumza na Watumishi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi hiyo jijini Dodoma Agosti 23, 2024 mara baada ya kufanya ziara ya kikazi ofisini hapo.*

Katika miaka ya karibuni, Serikali imekuwa ikisisitiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji na upokeaji huduma. Matumizi ya mifumo yamekuwa nyenzo muhimu hasa wakati huu wa ukuaji wa sayansi na teknolojia kwani yanarahisisha upatinanaji na utoaji huduma na kuondoa uwezekano wa mtoa huduma na mpokea huduma kukutana uso kwa uso.

Matumizi haya pia yameondoa mikutano na mazungumzo yaliyokuwa yakifanyika wakati wa upokeaji na utoaji huduma na kurahisisha mawasiliano, kuleta ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli mbalimbali serikalini.

Kutokana na sababu hiyo, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma tangu mwaka 2023, ilijenga mfumo wa kuwawezesha Viongozi wa Umma kujaza na kuwasilisha kwa Kamishna wa Maadili Tamko la Rasilimali na Madeni kwa urahisi.

Kuanza kwa matumizi ya Mfumo wa Ujazaji na Utoaji Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya Mtandao (Online Declaration System – ODS) ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali yanayozitaka Wizara, Idara na Taasisi za Umma kutoa huduma kwa kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuwapunguzia adha wananchi. ODS inamuwezesha Kiongozi wa Umma kujaza na kuwasilisha Tamko lake kwa njia ya mtandao akiwa popote duniani mtandao unapopatikana. Viongozi wa Umma wanaingia katika Mfumo wa ODS kwa kutumia anuani ya https://ods.maadili.go.tz au kupitia tovuti ya taasisi yenye anuani www.maadili.go.tz na kubonyeza kitufe chenye neno 'ODS.'

Jumla ya Viongozi wa Umma 15,480 kati ya 15,903 walirejesha Tamko lao la mwaka 2024 kwa Kamishna wa Maadili kwa njia ya mtandao. Kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398, kiongozi wa umma kila ifikapo tarehe 31 Desemba ya kila mwaka hulazimika kuwasilisha Tamko la Rasilimali na Madeni kwa Kamishna wa Maadili. Kabla ya kuanzishwa kwa ODS,

*Inaendelea UK... 15*

# Mfumo wa ODS furaha kwa viongozi

Sekretarieti ya Maadili ilikuwa ikichapisha nakala za Tamko na kuwatumia viongozi ili wajaze kwa mkono, kisha kuwasilisha kwa Kamishna wa Maadili nakala ngumu (hard copy). Njia hii iliwagharimu sana viongozi na taasisi kwa kutumia fedha na muda mrefu kujaza tamko na kuliwasilisha katika ofisi za Sekretarieti.

Aidha, Sekretarieti ilikuwa ikitumia kati ya shilingi milioni 35 hadi 40 kwa mwaka kuchapisha fomu za Tamko. Awali, viongozi walilazimika kutembea umbali mrefu kuwasilisha matamko yao ama Makao Makuu ya taasisi au katika ofisi zake za kanda au kuwasilisha matamko hayo kwa njia ya Posta.

Sekretarieti ya Maadili inazo jumla ya ofisi Nane tu nchini. Ofisi hizo ni Kanda ya Mashariki (Morogoro), Kanda ya Magharibi (Tabora), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Kusini (Mtwara), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda Maalum (Dar Es Salaam) na Kanda ya Kaskazini (Arusha).

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Clement Sangu (Mb) wakati wa ziara yake katika ofisi za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu Dodoma kabla ya kuanza kwa zoezi la urejeshaji wa Tamko la mwisho wa mwaka 2024, aliunga mkono matumizi ya mfumo huo na kusisitiza kuwa uwe wa kudumu na endelevu.

"Mmeandika hapa kuhusu baadhi ya Viongozi kuwa na wasiwasi na mfumo kuhusu taarifa zao, wasiwasi wa nini kwenye jambo lenye maslahi ya Umma! Hatuwezi kufanya kazi kwa kufuata hisia ama kumridhisha Kiongozi fulani, jambo la nyumbani kwako ndio uwe na wasiwasi nalo, kama Sekretarieti wamesema wote twende online basi ni online," alisisitiza Mhe. Sangu.

Mhe. Naibu Waziri aliongeza kuwa, "njia hii ni nzuri sana kuliko hayo makaratasi, maana mfumo huu utawasaidia kumaliza matatizo yote na kuchambua hizo sampuli kwa haraka zaidi na kwa wakati kuliko mfumo wa awali ambapo karatasi mpaka zifike Sekretarieti mnajikuta mmetumia nguvu na gharama kubwa."

Katika hatua nyingine, Mhe. Sangu aliiagiza Sekretarieti kubuni utaratibu wa viongozi wa umma kujaza Tamko wakati wowote wanapoongeza au kupunguza mali badala ya kusubiri mwishoni mwa mwaka.

"Jambo hili lisiishie tu hapa, naomba jambo hili liwe la kudumu na liendelee mwaka mzima wa bajeti kwani kwa sasa tumeshatoka huko katika Dunia ya 'Manual' kila kitu kinakwenda mtandaoni," aliongeza Mhe. Sangu.

Akitoa elimu kwa wageni mbalimbali waliotembelea banda la Sekretarieti ya maadili katika Maonesho ya Kitaifa ya Sikukuu ya Wakulima Nane Nane Agosti, 2024, jijini Dodoma, Katibu idara ya Ukuzaji Maadili kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Bw. Waziri Kipacha alisema ODS ilianzishwa kuwapunguzia viongozi kadhia ya kusafiri umbali mrefu kuwasilisha nakala za Tamko kwa Kamishna wa




*Inaendelea UK..16*



**Afisa kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Bi Modesta Mtui, akitoa maelezo juu ya mfumo wa ujazaji wa matamko ya rasilimali na madeni ya viongozi kwa njia ya mtandao kwa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mhe. Remidius Mwema katika maonesho ya sikukuku ya wakulima (Nanenane) yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma, tarehe 6 Agosti, 2024**

*Inatoka UK..15*

Maadili, kupunguza gharama za uendeshaji na kuondoa msongamano wa Viongozi wa Umma waliokuwa wakija kwa wingi katika ofisi za Sekretarieti kuwasilisha matamko yao.

"Mfumo wetu wa ODS, unafanya kazi popote mtandao wa 'internet' unapopatikana, hivyo hakuna ulazima wa kiongozi kufika katika ofisi zetu kuwasilisha Tamko, maana mhusika anauwezo wa kujaza taarifa zake akiwa popote pale na pia ni rahisi kiongozi kutunza taarifa zake, " alisema Bw. Kipacha.

"Viongozi wamekua wakitumia gharama kubwa kujaza matamko yao kwa kutumia mfumo wa nakala ngumu, hivyo mfumo huu wa kujaza matamko mtandaoni utapunguza gharama hizo na pia zoezi hilo litatumia muda mfupi kukamilika," aliongeza Bw. Kipacha.

Aidha, Bw Kipacha alisema, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imekuwa ikitoa elimu kwa Viongozi kwa njia mbalimbali kuhusu ODS ili kufanikisha malengo ya kuanzisha mfumo huo.

"Sisi kazi yetu ni kutoa elimu kwa jamii na Viongozi wa Umma kuhusu ODS. Hivyo, katika kukamilisha azma hii, tumetumia njia mbalimbali ikiwemo vipeperushi kwa Viongozi wa Umma na wadau wetu wengine kuelezea mfumo huu. Njia hii imesaidia kufikisha ujumbe haraka kwa viongozi kuhusu ya ODS," alisisitiza.

Njia nyingine iliyotumika kuutarifu umma kuhusu mfumo huu mpya wa upokeaji wa matamko ni vyombo vya habari, ikiwemo mitandao ya kijamii na machapisho mbali mbali. "Mfumo wa ODS una namna ya kutoa maelekezo kwa mtumiaji kwa jinsi gani anaweza kukamilisha taarifa zake, cha msingi awe amejisajili."

"Kwa viongozi ambao tayari wameshajisajili kwenye mfumo, mfumo wenyewe una sehemu inayotoa maelekezo kwa mtumiaji hasa namna ya kujaza taarifa zake muhimu," aliongeza Bw. Kipacha.

Akizungumzia mfumo huo, Mkuu wa Wilaya ya Kiteto iliyopo Mkoani Manyara, Mhe Remidius Mwema alielezea kufurahishwa kwake na uanzishwaji wa ODS na jinsi inavyomsaidia kiongozi kufanyakazi kwa urahisi akiwa mahali popote anaweza kujaza taarifa zake na kisha kuendelea na majukumu mengine akiwa ofisini kwake.

"Nina furaha kwa kuletwa mfumo huu maana naweza kuwa ofisini na kisha kutenga muda mchache kwa ajili ya kujaza taarifa zangu 'online' (mtandaoni) huku nikiendelea na majukumu mengine ya kuwahudumia wananchi," alisema Mhe. Mwema.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya ya Kiteto, licha ya mfumo wa ODS kuondoa gharama hasa upande wa usafiri na kutuma kwa njia ya posta pia mfumo umesaidia kutunza taarifa za kiongozi husika, hivyo kufanya wepesi katika kupata kumbukumbu za taarifa za awali.

# HABARI PICHA



*Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mhe. Queen Sendiga (aliyeketi upande wa kulia) akishuhudia Kiapo cha Ahadi ya Uadilifu kwa Mhe. Michael John Semindu, Mkuu wa Wilaya ya Mbulu. Kiapo hicho kiliongozwa na Katibu Msaidizi Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Kanda ya Kaskazini  Arusha Bw. Gerald Mwaitebele (katikati) tarehe 29 Januari, 2025 mkoani Manyara.*




*Katibu Idara ya Usimamizi wa Maadili, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Bw. Kassim Mkwawa, akitoa cheti cha ushiriki wa mafunzo ya awali kwa Bw. Haji Tawah ambaye ni mtumishi wa Ofisi hiyo. Zoezi hilo lilifanyika Makao Makuu ya ofisi hiyo jijini Dodoma tarehe 13 Novemba, 2024.*

# Viongozi wapigwa msasa wa Maadili

Inatoka UK..11

umma wasio waadilifu, wamekuwa wakijihusisha na vitendo vinavyopelekea uwepo wa mgongano wa maslahi kati yao na Taasisi wanazozisimamia na kwamba suala hili linapunguza kasi ya ukuaji wa uchumi na kurudisha nyuma juhudi za serikali za utoaji huduma kwa jamii," alisema.

Aidha, Mhe. Mtambi alitoa rai kwa viongozi wa umma mkoani Mara, kuzingatia matakwa ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ikiwemo ujazaji wa Tamko la Raslimali kila ifikapo tarehe 31 Desemba, kuzingatia uwajibikaji wa pamoja, kuwa wawazi na kujiepusha na matumizi mabaya ya madaraka.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Martin Shigella alibainisha kuwa mafunzo ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yatawasaidia viongozi mkoani kwake kubadilika katika tabia na mienendo yao na kutimiza majukumu kwa uadilifu.

"Mafunzo haya ni msaada mkubwa sana kwetu hasa matumizi ya teknolojia katika kuzingatia takwa la kisheria la kujaza tamko tukiwa popote pale bila kutumia muda mrefu kusafiri kutoka Mkoa mmoja hadi mwingine zilipo ofisi za Sekretarieti ya Maadili kupeleka tamko."

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo ambaye ni Diwani wa Kata ya Nyamrandirira Wilaya ya Musoma, Mhe. Wanjara Nyaoja aliipongeza Sekretarieti ya Maadili kwa kutoa mafunzo yanayowasidia viongozi kuijua Sheria ya Maadili ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka na mgongano wa maslahi.



*Afisa kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati Dodoma Bw. Joshua Mwambande akitoa mada kuhusu maadili kwa Waheshimiwa Madiwani na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Manispaa ya Singida katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Mwenge tarehe 23 Januari, 2025.*

"Nashauri utaratibu huu wa kutupatia elimu ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma uwe endelevu kwasababu unatusaidia kujua mipaka yetu na kushirikiana kuwahudumia wananchi," alisema.

Naye Katibu Msaidizi, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Ziwa Bw. Godson Kweka akiongea katika mafunzo hayo, alisema kuwa mkakati wa utoaji wa elimu ya Uwajibikaji wa Pamoja kwa Viongozi wa Umma nchini, ni endelevu na unalenga kuwapatia elimu ya maadili viongozi katika maeneo yao ya kazi.

"Lengo ni kuwakumbusha viongozi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na wajibu wao katika utekelezaji wa ma-jukumu yao wanapowahudumia wananchi," alisema na kuongeza kuwa, "Viongozi wa Umma wanatakiwa kuijua misingi ya maadili na kujiepusha na mgongano wa maslahi kwa sababu suala hili linapigiwa kelele sana katika jamii yetu."

Bw. Kweka aliwataka Viongozi wa Umma kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi na kutanguliza maslahi ya umma mbele, kujiepusha na vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma.

Tathmini iliyofanywa na Sekretarieti ya Maadili katika Halmashauri za Wilaya zilizopatiwa elimu ya Uwajibikaji wa Pamoja, inaonesha kuwa karibu Halmashuri zote imeanza kutengamaa na viongozi wengi wameelewa majukumu na mipaka yao ya kazi.

# HABARI PICHA



***Baadhi ya Watumishi Wanawake wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu na Kanda ya Kati wakiwa katika picha ya pamoja katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma tarehe 8 Machi, 2025.***



***Kamishna wa Maadili Mhe. Jaji (Stahiki) Sivangilwa Mwangesi (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Baraza hilo lilifanyika Makao Makuu ya ofisi hiyo jijini Dodoma tarehe 12 Machi, 2025.***

# HABARI PICHA



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Mhe. Yagi Maulid akifungua mafunzo ya Maadili kwa Waheshimiwa Madiwani na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Manispaa ya Singida yaliyofanyika katika ukumbi wa  Shule ya sekondari Mwenge tarehe 23 Januari, 2025. Mafunzo hayo yameandaliwa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kushoto ni Naibu Meya Mhe. Gwae Mbua na kulia ni Mkurugenzi wa Manispaa, Bi. Joanfaith Kataraia.*



*Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma wakifuatilia mada kuhusu umuhimu wa Klabu za Maadili mashuleni kutoka kwa Afisa wa Sekretarieti ya Maadili Bw. Joshua Mwambande (hayupo pichani) katika ukumbi wa shule ya sekondari Mpwapwa tarehe 25 Aprili, 2025.*

# Mafanikio ya Miaka Minne ya Dkt. Samia

Inatoka UK..13

Viongozi wa Umma waliokuwa wakilalamikiwa kukiuka Sheria na kujengewa misingi ya uadilifu katika ngazi ya chini kupitia Klabu za Maadili.

**Uendeshaji wa Baraza la Maadili**

Kulingana na muundo wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Baraza la Maadili ni chombo cha mwisho katika kufanya maamuzi kuhusu masuala ya ukiukwaji wa maadili miongoni mwa Viongozi wa Umma. Baraza la Maadili lina jukumu la msingi la kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma au malalamiko yaliyofanyiwa uchunguzi wa awali na Sekretarieti ya Maadili. Katika Awamu ya Sita, Baraza limefanya uchunguzi wa kina wa malalamiko 23 yaliyowasilishwa mbele yake na Sekretarieti ya Maadili. Malalamiko hayo yaliwahusu Viongozi wa Umma kutoka Taasisi mbalimbali za Umma. Malalamiko yaliyofikishwa mbele ya Baraza la Maadili katika Awamu ya Sita ni mengi kuliko malalamiko yaliyowahi kusikilizwa katika awamu moja tangu kuanzishwa kwa Taasisi. Viongozi husika walituhumiwa kwa makosa mbalimbali ikijumuisha; matumizi mabaya ya madaraka; kuwa na mgongano wa maslahi, matumizi ya vitisho, matusi na kushindwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika utendaji kazi. Baada ya kufanya uchunguzi wa kina, Baraza hutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa kwa viongozi waliokutwa na hatia.

**Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA.**

Sekretarieti ya Maadili imehama kutoka katika matumizi ya mfumo wa karatasi (manual system) na kuanza matumizi ya TEHAMA katika kupokea, kuchambua, kuhifadhi taarifa na kumbukumbu mbalimbali kutoka kwa Viongozi wa Umma kuhusu mali, madeni na malalamiko ya ukiukwaji wa maadili. Katika Awamu ya Sita, Sekretarieti ya Maadili imeanzisha matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili (Ethics Management Information System - EMIS). Mfumo huu, unarahisisha uchambuzi na upatikanaji wa taarifa za kimaadili ili kutoa maamuzi kwa wakati. Aidha, mfumo unarahisisha ukusanyaji, uchakataji, utunzaji wa taarifa na kumbukumbu mbalimbali kuhusu malalamiko ya ukiukwaji wa maadili.

Aidha, Sekretarieti ya Maadili imejenga Mfumo wa ujazaji Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao "Online Declaration System – ODS." Mfumo huu umeondoa utaratibu wa zamani wa viongozi wa umma kujaza matamko yao kwa kutumia karatasi. Mfumo unawawezesha viongozi wa umma kujaza tamko na kuliwasilisha kwa Kamishna wa Maadili wakiwa mahali popote penye mtandao. Matumizi ya ODS yamewaondolea viongozi wa umma adha ya kusafiri mwendo mrefu kuwasilisha matamko katika ofisi za Sekretarieti ya Maadili.

Jumla ya Viongozi wa Umma 15,480 waliwasilisha Tamko la Rasilimali na Madeni la mwisho wa mwaka Desemba 31, 2024 kwa njia ya ODS.

**Uboreshaji Miundombinu ya Ofisi na Vitendea Kazi**

Katika kipindi cha Awamu ya Sita ya uongozi, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2020 Ibara ya 112 kwa kuboresha miundombinu na vitendea kazi ili kuleta ufanisi wa kazi. Katika kutekeleza takwa hili, Sekretarieti imekamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi za Maadili Makao Makuu na Ofisi za Kanda ya Kati-Dodoma na kuhamia. Aidha, Sekretarieti imeanza ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Ziwa (Mwanza) ambalo kwa sasa umefikia asilimia 28.

**Scan kusoma Jarida Kidijitali**




*Muonekano wa Jengo la Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu na Kanda ya Kati-Dodoma zilizopo 1 Mtaa wa Maadili, 41104 Tambukareli jijini Dodoma.*



*Wajumbe wa Menejimenti wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wakitoa Ahadi ya Uadilifu mbele ya Afisa kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Bi. Deborah Mwanjali, Ahadi ya Uadilifu hiyo imetolewa tarehe 11 Machi, 2025 katika Ofisi za REA jijini Dodoma.*

# HABARI PICHA NA MAWASILIANO



***Afisa kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati Bw. Christian Kapere akitoa elimu ya Maadili kwa wanachama wa Klabu ya Maadili ambao ni wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwasi Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, Kanda ya Kati inaendelea na zoezi la kuhuisha na kufungua Klabu mpya za Maadili katika Shule za Msingi na Sekondari, zoezi hilo lilifanyika tarehe 23 Aprili, 2025.***

# MAWASILIANO

**MAKAO MAKUU**
1 Mtaa wa Maadili
41104 Tambukareli
S.L.P 225,
DODOMA
Simu: +255734101040 AU +255262160199

**KANDA YA KATI**
Mikoa ya Dodoma na Singida
1 Mtaa wa Maadili
41104 Tambukareli
S.L.P 1887 Dodoma,
Baruapepe:dodoma@maadili.go.tz
Simu: +255 26 232 1059

**KANDA YA ZIWA**
Mikoa ya Geita, Kagera, Mara na Mwanza
S.L.P 1473 Mwanza
Mt Kenyatta
Jengo la NSSF,
Baruapepe:mwanza@maadili.go.tz
Simu: +255 28 2505005

**KANDA MAALUMU**
Mikoa ya Dar ea Salaam, Pwani na Zanzibar
Jengo la Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili, Mtaa wa Ohio.
S.L.P 13341, Dar es Salaam.
Barua pepe:dsm@maadili.go.tz
Simu: +255 22211810


**KANDA YA MAGHARIBI**
Mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga na Simiyu
S.L.P 1126 Tabora,
Ofisi ya Kilimo, Br. Boma
Baruapepe:tabora@maadili.go.tz
Simu: +255 26 2605322

**KANDA YA MASHARIKI**
Mikoa ya Morogoro na Tanga
S.L.P 212 Morogoro,
Jengo la Mafao NSSF,
Baruapepe:morogoro@maadili.go.tz
Simu: +255 23 2613741

**KANDA YA KASKAZINI**
Mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro
Jengo la Hazina
S.L.P 3174, Arusha,
Baruapepe:arusha@maadili.go.tz
Simu: +255 272970774

**KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Rukwa Songwe na Katavi
Jengo la NHIF,
S.L.P 6311, Mbeya.
Baruapepe:mbeya@maadili.GO.TZ
Simu: Simu: +255 25 250 2714

**KANDA YA KUSINI**
Mikoa ya Lindi, Mtwara and Ruvuma
S.L.P 218, Mtwara,
Mt. Chikongola , Barabara ya TANU
Baruapepe:mtwara@maadili.go.tz
Simu: +255 23 23233963




Scan kusoma
Jarida Kidijitali

Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, 1 Mtaa wa Maadili, 41104 Tambukareli, S.L.P 225, DODOMA Simu: +255734101040 AU +255262160199